لا إله إلا الله محمد رسول الله

JIUNGENI NA

# JUMUIYA YA WAISLAMU

## YENYE IMAMU



SHEIKH MUZAFFAR AHMAD DURRANI

JUMUIYA YA WAISLAMU
WAAHMADIYYA TANZANIA

**Jiungeni na Jumuiya ya Waislamu Yenye Imam**

**Mwandishi: Sheikh Muzaffar Ahmad Durrani**

**ISBN 9987-8932-7-9**

**© Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya Tanzania**

| | |
|---|---|
| **Chapa ya Kwanza na Pili** | **Nakala 24,000** |
| **Chapa ya Tatu Septemba 2002,** | **Nakala 20,000** |
| **Chapa ya Nne Januari 2008,** | **Nakala 10,000** |

**Kimeenezwa na:**
**Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania**
**S.L.P. 376 - Dar es Salaam**
**Simu: 00255 -22- 2110473 Fax: 00255 -22-2121744**

**Kimepigwa chapa na:**
**Ahmadiyya Printing Press**
**S.L.P. 376, Dar es Salaam**
**Tanzania**

بِسْمِ اللهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ

***Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu***

Sayyidna Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s. (1835 - 1908 A.D.) Mwanzilishi Mtukufu wa Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya ametumwa na Mwenyezi Mungu kwa niaba ya Mtukufu Mtume Muhammad s.a.w. kuimarisha Dini ya Kiislam. Alidai kwamba yeye ni Imam Mahdi na Masihi Aliyeahidiwa na Mtume Mtukufu Muhamamd s.a.w. na yeye ndiye kiongozi wa zama hizi. Wafuasi wake walipatikana katika Afrika mashariki zama za uhai wake mnamo mwaka 1896 A.D. Yeye aliimarisha na alifundisha dini ya Kiislaam, ile ile iliyoletwa na Mtume Muhammad s.a.w.

Baada yake makhalifa wake wamekuja sawa na ahadi ya Mwenyezi Mungu na utabiri wa Mtume Mtukufu s.a.w. (Quran 24:56; *Musnad Ahmad Jal. 4 uk. 273, Mishkat Bab Indhar).* Kazi za Jumuiya na nidhamu ya Jumuiya inapendeza, huduma ya kuimarisha Dini ya Kiislam na kueneza mafundisho yake ni ya kutosheleza na hivyo ndivyo inavyotakiwa.

## SHABAHA YA KUANZISHA JUMUIYA MPYA

Sasa swali laweza kuzuka kwamba, wakati Seyyidna Ahmad a.s. alitumwa kuimarisha Dini ya Kiislam, ni kwa nini hakuungana na Waislam wengine, badala yake akaanzisha Jumuiya mpya na kujitenga nao?

**JIBU:**

1.Utabiri ulikuwepo wa Mtume Muhammad s.a.w. kwamba, wakati Waislamu watagawanyika makundi 73, yote yataingia motoni isipokuwa kundi moja pekee ndilo litaenda Peponi. *(Jamee Tirmidhi Baabu Iftiraq).* Aliulizwa ni kundi gani hilo? Akasema Jamaat - yaani Jumuiya. Hivi ilikuwa lazima sawa na utabiri, Jumuiya ile ingepatikana. Kwa nia

hii na kwa idhini ya Mwenyezi Mungu Seyyidna Ahmad a.s. alianzisha Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya.

2. Seyyidna Ahmad a.s. ndiye Imam wa zama hizi. Jemedari wa jeshi la kiroho. Wakati yeye ameitwa Imam ni lazima awe na wafuasi wake, Wakati yeye ni Jemedari wa jeshi la kiroho lazima awe na jeshi la Dini. Yeye alitengeneza lile Jeshi la Mungu linaloitwa Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya.

3. Wakati Sayyidna Ahmad a.s. alitumwa kuhuisha Dini ya Kiislamu. Je, angefanya kazi peke yake? Taratibu ya kazi inakuwa hivi kwamba kiongozi anaongoza na wafuasi wake na wadogo wake wanafuata na wanafanya kazi. Sasa angalieni wakati Imam Mahdi angetaka kuchapisha Qurani na Hadithi, angewaambia nani kazi hii? Wakati angetaka kujenga msikiti na madrasa angemwambia nani? Wakati angetaka kuwaita watu mkutanoni angewaita nani? Wakati angetaka kuwatuma wabashiri nchi za nje angewatuma nani? Jibu la maswali hayo na mengineyo ni kwamba lazima awe na wafuasi wake, wale ambao wanajulikana, wale ambao wanamfuata, na lazima wawe na jina lolote.

## JINA LA JUMUIYA YA WAISLAM WAAHMADIYYA

Seyyidna Ahmad a.s. kwa idhini ya Mwenyezi Mungu tarehe 23/3/1889 A.D. alianza kupokea Bait za watu, na siku hadi siku watu maelfu walijiunga naye. Sasa swali lilikuwa hili kwamba watambulike kwa jina gani? Kwa sababu Waislamu walianza kujiita kwa majina mbalimbali. Kwa hiyo ilikuwa muhimu sana kwamba wafuasi wa Seyyidna Ahmad wawe na jina maalumu.
Seyyidna Ahmad a.s. ambaye alitumwa kwa niaba ya Mtume Mtukufu Muhammad s.a.w. yeye alisema kwamba yeye hana chochote ila cha Muhammad s.a.w. na wafuasi wake si mbali na wafuasi wa Mtukufu

Mtume Muhammad s.a.w. Hivyo aliwaita wafuasi wake kwa jina la Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya. Kwa sababu ya jina la pili - Ahmad - la Mtume Muhammad s.a.w.

Hapa ni vyema ieleweke vizuri kwamba jina la Ahmadiyya si kwa sababu ya jina la Ahmad a.s. mwanazilishi wa Jumuiya. Bali ni kwa sababu ya jina la pili la Mtume Mtukufu s.a.w. na muradi wake ni Waislamu wa Mtume Muhammad s.a.w. Si Waislamu wa katikati wala wa baadaye, kama vile wengine wajiitavyo kwa jina la Sheikh fulani au mwalimu yeyote.

## TOFAUTI BAINA YA WAISLAMU WAAHMADIYYA NA WAISLAMU WENGINE

Kama inavyoeleweka kwamba, Waislamu wote wanayo dini moja yaani dini ya Kiislamu. Nguzo za dini ya Kiislamu ni zilezile tano, na nguzo za imani ni zilezile sita. Wote wanamwamini Mwenyezi Mungu na Mtume wake Muhamamd s.a.w. Lakini baadhi ya wakati inaonekana hitilafu baina yao, ambapo wakati mwingine hitilafu hizi huwa kubwa mpaka baadhi ya Waislamu wanawadhania vibaya wengine. Katika kitabu hiki tunachukua fursa hii kueleza tofauti baina ya Waislamu wa Ahmadiyya na Waislamu wengine.

(1) Waislamu Waahmadiyya tunaamini itikadi zile tu zinazoelezwa katika Qurani na Hadithi za Mtume s.a.w. na tunakataa Bidaa na mambo yaliyobuniwa baadaye katika dini. (3:86).
Lakini Waislamu wengine wanaamini itikadi ambazo hazipatikani katika Qur'ani na Hadithi na hii ni tofauti ya msingi.
Kama mfano, Waislamu wengine wanaamini kwamba:

(2) Waislam wa Ahmadiyya tunaamini kwamba Mola wetu anazo sifa zote njema na hana mabadiliko katika sifa yake yoyote, na kazi zote anafanya alizokuwa akifanya zamani.
Lakini Waislamu wengine wanaamini kwamba Mwenyezi Mungu haongei

na mtu yeyote siku hizi, hata kama mtu huyo awe na imani ya hali ya juu namna gani. Kana kwamba Mungu wao siku hizi ni bubu na anakosa sifa moja ya kuongea.

(3) Waislamu wa Ahmadiyya tunaamini kwamba Malaika ni viumbe wa Mwenyezi Mungu na wanafanya kazi chini ya mwongozo wa Mwenyezi Mungu na kazi yao moja ni kuleta Wahyi (ufunuo) kwa watu wema wa Mungu na bado wanaendelea kufanya kazi hii kama Mwenyezi Mungu anavyoeleza katika Qurani Tukufu (41:31-32; 97:5-6).
Lakini Waislamu wengine wanasema kwamba Malaika hawafanyi kazi hii siku hizi bali wamekaa bure tu.

(4) Waislamu wa Ahmadiyya Tunaamini kwamba Qurani Tukufu ni kitabu cha Mwenyezi Mungu ambacho hakina shaka yoyote ndani yake wala hakuna mabadiliko wala mafutiko katika Qurani, kwa sababu Mwenyezi Mungu ni mlinzi wake (15:10).
Lakini Waislamu wengine wanaamini kwamba aya kadhaa za Qurani tukufu zimebadilika na zingine hazina athari zao na zingine zimefutwa, wanaziita kwa maneno ya Naasikh na Mansuukh. Wengi wao hawaiamini *Bismillahir Rahmaanir Rahiim* kuwa ni aya ya kwanza ya kila sura iliyowekwa juu yake.
(5) Waislamu Waahamdiyya tunaamini kwamba Mitume wote wa Mwenyezi Mungu hawana dhambi yoyote. Wote walikuwa wapendwa wa Mwenyezi Mungu na wenye utawa na uchamungu.
Lakini Waislamu wengine wanahitilafiana nasi, wanasema kwamba Mitume walikuwa na dhambi kama vile kusema uongo, kuelekea kwa wanawake wengine na kadhalika. Mifano mingi ya aina hii imetajwa katika tafsiri zao za Qurani hata mingine kumhusu Mtume Mtukufu Muhammad s.a.w. *(nau'udhu billahi min dhaalika)*. Angalia Tafsiri ya Jalalain maelezo ya Aya ya 24 Surat Yunus na pia maelezo ya aya ya 37 Suratul Ahzaab.

(6) Waislamu wa Ahamdiyya tunaamini kwamba Hadhrat Isa a.s. (Yesu

Kristo) alikuwa Nabii wa Mwenyezi Mungu tu. Akiwa mwanadamu alikufa kifo cha kawaida kama walivyokufa Mitume wengine wa Mwenyezi Mungu. (3:145 na 5:76) na hana sifa yoyote ya Mungu kama kuishi bila kula chakula. Mayahudi walishindwa kumfisha msalabani (kumsulubu) bali Mwenyezi Mungu alimsaidia na kumlinda na kifo cha msalaba na baada ya mateso aliyoyapata msalabani alihamia nchi za Mashariki, akaishi huko na kufia huko katika umri wa miaka 120 *(Kanzul Ummal* Jl. 6 Uk. 160).
Lakini Waislamu wengine wanawaunga mkono Wakristo kusema kwamba Nabii Isa a.s. yu mzima mbinguni pamoja na Mwenyezi Mungu! Anaishi huko bila kula chakula na bila mahitaji mengine ya kibinadamu na hana mabadiliko. Kana kwamba ni Mungu wao mdogo.

(7) Sisi Waislamu wa Ahmadiyya tunaamini kwamba utume ni neema na baraka ya Mwenyezi Mungu na neema zake zinahitajika kwa mwanadamu kwa ajili ya maendeleo yake ya kiroho. Muongozo wake unahitajika wakati ugonjwa wa kiroho unapotokea kama vile dawa inavyohitajika wakati ugonjwa wa kimwili unapotokea. Hivyo sisi tunaamini kwamba utume katika dini ya Kiislamu (kwa wafuasi wateule wa Mtukufu Mtume s.a.w.), unaendelea . Kazi ya Mitume hao ni kufundisha na kueleza aya za Mwenyezi Mungu na kuelekeza kwenye dini ileile iliyofundishwa na Mtume Muhammad s.a.w. (7:36). Kwa kuthibitisha hili amekuja Hadhrat Ahmad a.s. Mwanzilishi wa Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya, kutoka kwa Mwenyezi Mungu kwa niaba ya Mtume Muhamamd s.a.w. Hii ni kweli kabisa kwamba dini ya Kiislamu imekamilika, sasa hakuna dini nyingine ila Islam, na Mtume yeyote hana nafasi ya kuja kupinga au kubadilisha mafundisho ya dini ya Kiislamu. Yeyote atakayetumwa lazima awe mtumishi na mfuasi wa Mtume Mtukufu Muhammad s.a.w.
Lakini Waislamu wengine wanasema kwamba Mtume Muhamamd s.a.w. ni Mtume wa mwisho, na neema yoyote haitapatikana katika umati wake. Balaa, fitina uwongo, udanganyifu, kugawanyika, madajjali, vyote vitapatikana lakini dawa au mtu wa Mungu hatakuja.

Ingawaje Waislamu hawa wakati mwingine wanajipinga na kuhisia haja ya mtu wa Mungu pale wanaposema kwamba Nabii Isa a.s. atashuka kutoka mbinguni kwa ajili ya kuwaongoza Waislamu kwenye ushindi. Hawataki kabisa kwamba mwana (mfuasi) wa Muhamamd s.a.w. achaguliwe kutuongoza lakini wanamtegemea mwana wa Israeli aje kuuhukumu umati wa Muhamamd s.a.w. Wao bila kujijua, maskini, wanaikana nguvu ya kiroho ya kutakasa ya Mtume wao Mtukufu s.a.w.!

(8) Waislamu wa Ahamdiyya tunaiamini ahadi ya Mwenyezi Mungu aliyowaahidi waaminio katika Qurani (24:56) kwamba wale watakaoamini na kufanya vitendo vizuri watafanywa Makhalifa katika ardhi.
Sawa na ahadi hii ya Mwenyezi Mungu yeye tayari ameshaleta Makhalifa kati ya Wasialmu ili kutimiza ahadi yake. Na kwa fadhili zisizo kikomo za Mwenyezi Mungu Jumuiya ya Waislamu wa Ahamdiyya inaongozwa na Khalifa.
Lakini Waislamu wengine wanasema kwamba siku hizi hakuna Khalifa kati ya Waislamu na Waislamu wote wanaishi bila kiongozi yeyote. Yaani umati hauna baba kama mwili usio na kichwa. Tunawauliza Je, Mungu wao amesahau ahadi yake au wao wamekosa imani??

(9) Mtume Mtukufu Muhamamd s.a.w. alitabiri kwamba baada ya kila miaka mia moja Mwenyezi Mungu atamuinua Mujaddid (Mwenye kuimarisha dini) (Abu Daudi, Kitaabul Fitan).
Tunaamini kwamba sawa na utabiri wa Mtume Mtukufu s.a.w. katika kila karne ya Kiislamu Mujaddid walifika na Mujaddid wa karne ya 14 ni Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s.
Waislamu wengine wameanzisha dhana kwamba Mwenyezi Mungu aliendelea kuwaleta Mujaddid mpaka karne ya 13 lakini katika karne ya 14 Mwenyezi Mungu hakuleta Mujaddid yeyote. Sasa ni karne ya 15 ya Kiislamu.

(10) Mtume s.a.w. alitabiri kwamba wakati wa upotevu wa umma wake

Masihi na Mahdi atakuja kuwaongoza Waislamu na kuleta ushindi wa dini ya Kiislamu.
Sasa Waislamu Waahmadiyya tunaamini kwamba katika wakati huu wa upotevu wa umma wa Mtume s.a.w. Mwenyezi Mungu amemtuma Masihi Aliyeahidiwa na Imam Mahdi ambaye ni Seyyidna Ahmad a.s. Lakini Waislamu wengine wanasema kwamba hii ni kweli upotevu na mfarakano mkubwa umetokea katika Waislamu, lakini kiongozi wa kidini, Imam wa Kiroho hajapatikana. Ugonjwa umeenea sana lakini dawa haijapatikana. Kama waulizwe, je, Mtume wenu alisema kweli, au Mungu wake hakutambua ahadi aliyowapa wafuasi wake? Watajibuje!!!

(11) Sisi Waislamu wa Ahamdiyya tunaamini kwamba dini ya Kiislamu ilikamilika katika maisha ya Mtume Muhamamd s.a.w., na baada yake mtu yeyote hana ruhusa kuongeza wala kupunguza chochote katika sheria za Kiislamu. Wakati tunatangaza dini halisi bila bidaa yoyote Waislamu wengine wanafikiri kwamba tunatangaza dini mpya. Ilhali hawa jamaa wameifunika dini na takataka nyingi za bidaa. Hivyo wanapoelezwa dini halisi ya Mtume Muhamamd s.a.w. wanafikiri kuwa ni dini mpya.
Kwa mfano mambo kama:
(i) Khitima, (ii) Arobaini, (iii) Talasimu, (iv) Talaqini, (v) Maulidi ya kupiga ngoma na kucheza dansi na kadha wa kadha, ilhali mambo haya yote hayana msingi katika dini, si suna ya Mtume s.a.w. Mtukufu wala ya Masahaba wake, Bali wametunga mambo haya baadaye kwa matamanio yao.

12. Sisi Waislamu wa Ahmadiyya tunaamini kwamba Hadhrat Muhammad s.a.w. ndiye Khaatamunnabiyyin. Yaani Mbora na Muhuri wa Manabii wote, na hatakuja Mtume yeyote baada yake ambaye aje na dini mpya au afundishe jambo lolote kinyume cha Sunna za Mtume s.a.w. Na tunaamini kwamba sasa daraja zote za kiroho zinapatikana katika umati wake. Waaminio wake na wafuasi wake watachaguliwa kwa kupewa neema zote.(4:70).

Lakini Waislamu wengine wanasema kwamba wafuasi wa Mtume Muhammad s.a.w. hawatapewa neema yoyote kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Bali Nabii Isa a.s. atakuja mara ya pili. Kwa njia hii sawa na jamaa hawa Nabii Isa a.s. ndiye mwisho wa Manabii na si Mtume Muhammad s.a.w., kwa sababu Nabii Isa a.s. sasa atakuja baada ya Muhammad s.a.w. na atafanya kazi ya utume baada ya Muhammad s.a.w. Baadhi yao wengine kwa kuona ubaya wa imani yao hiyo wanajasiri kiasi hiki kwamba wanasema Nabii Isa a.s. atakapokuja atanyang'anywa cheo chake cha Utume.

Sasa kila mtu anao uhuru wa kufuata imani yake. Kama wewe unaunga mkono upande wa juu basi wewe ni Muislamu Waahmadiyya, wewe ni ndugu yetu, uko wapi? Tunakutafuta.

Na mtu ambaye anaunga mkono upande wa chini, anakuwa upande wa hao Waislamu wengine. Pia kama wewe unakubaliana na mawazo ya Waislamu wengine chini ya kila nukta iliyoelezwa hapo juu, tunakukaribisha tafadhali uchunguze, uhakikishe kwamba ukweli uko wapi? Ili uweze kufuata Dini ya Mwenyezi Mungu na njia iliyonyooka.

**SWALI:**

Sayyidna Ahmad a.s. ametumwa na Mwenyezi Mungu, sawa, kwa nini anaongeza ongeza madai yake kama mfano kuwa Mujaddid, Mahdi, Masihi, Nabii, Rasuli na kadhalika.

**JIBU:**

1. Mitume wanachaguliwa na Mwenyezi Mungu na wanapewa madaraka na vyeo mbalimbali. Kwa hiyo wakati wanapewa madaraka yoyote, inakuwa ni jukumu lao kutangaza. Basi wanatangaza na wanadai madai yale wanayopewa na Mwenyezi Mungu.
2. Mitume hawafunuliwi mambo yote katika siku moja, bali wanaendelea kufunuliwa maisha yao yote. Basi jambo wanaloambiwa kwanza wanalitangaza kwanza, na jambo wanaloambiwa baadaye wanalitangaza baadaye. Kwa mfano Qur'an Tukufu iliteremshwa katika muda wa miaka 23.

3. Ulikuwepo utabiri wa kuongeza madai:
Imam Mahdi atadai kuwa Adam, Nuhu, Musa, Isa na Muhammad s.a.w. na Maimamu wa Ahlul Bait. *(Biharul Anwar* Jl. 13 uk. Na. 33).
4. Kuongeza ongeza madai ni sunna ya Mtume wetu Muhammad s.a.w inayopatikana katika Qur'an tukufu, Kwa hiyo Sayyidna Ahmad a.s. kwa sababu zilizotajwa hapo juu amejaaliwa kufuata nyayo na sunna za Mtume Mtukufu Muhammad s.a.w.

**Madai mbali mbali ya manabii katika Qur'an Tukufu**

**Mtume Muhammad s.a.w.**

1. Na siye Muhammad ila Mtume tu. (3:145).
2. Nabii aliye Ummi (7:158).
3. Nabii (33:2).
4. Shahidi (33:46).
5. Mubashshir (Mtoaji wa habari njema) (33:46).
6. Nazir (Muonyaji). (33:46).
7. Dai ila llah (Muitaji kwa Allah) (33:47).
8. Siraajumunira (Taa itoayo nuru (33:47).
9. Rehema kwa walimwengu (21:108).
10. Khaatamunnabiyyin (Muhuri wa Manabii) (33;41).
11. Muzammil (Mwenye kujifunika nguo) (73:2)
12. Mudaththir (Mwenye kuvaa) (74:2).

Madai, sifa na vyeo vya Mtume Mtukufu Muhammad s.a.w. vimetajwa vingi mno katika Qur'an Tukufu na katika Hadithi pia. Katika hadithi moja Mtume Mtukufu s.a.w. amesema: Mimi ni Muhammad, Ahmad, Mahi, Hasher na Aaqib. (Bukhari).
Vilevile manabii wengine pia walipewa vyeo mbalimbali. Tunawataja baadhi yao pamoja na vyeo vyao.

**Nabii Ibrahimu a.s.**
1. Swiddiq (19:42)
2. Nabii (19:42).

**Nabii Ismail a.s.**
1. Swadiqal Waa'di (Mkweli wa ahadi) 19:55).
2. Rasul (Mtume) (19:55).
3. Nabii (19:55)
4. Mardhiyya (Mridhiwa) (19:56).

**Nabii Mussa a.s.**
1. Mukhlaswan (Mteule) (19:62)
2. Rasul (Mtume) (19:52).
3. Nabii ( 19:52)

**Masihi Isa a.s.**
1. Masihi (4:173)
2. Isa (3:56).
3. Abdullah (19:31)
4. Nabii (19:31)
5. Mubarak (19:32)
6. Rasul (5:56).

## JIUNGENI NA JUMUIYA YENYE IMAM.

Mtume Mtukufu Muhammad s.a.w. ndiye Mwalimu kamili ambaye ametuelezea mambo yote yatakayotokea mpaka siku ya Kiyama. Kwa idhini ya Mwenyezi Mungu, alituelezea vizuri hatari ya mifarakano katika Dini ya Kiislamu na dawa yake. Sahaba mmoja Hadhrat Huzaifa Bin Yaman R.A anasimulia kwamba nilimuuliza Mtume Mtukufu s.a.w. kwamba tulikuwa katika upotevu na giza mpaka Mwenyezi Mungu

alikutuma. Sasa tumepata mwongozo na nuru. Je baada ya hayo tena tutapotea? Mtume Mtukufu s.a.w. alijibu ndiyo. Nilimuomba atueleze zaidi kuhusu upotevu huu. Alieleza kwamba wafalme wabaya watatawala, Waislamu watagawanyika, viongozi wao wataongoza kinyume na mwongozo wangu na watafundisha kinyume cha suna zangu. watakuwa mashetani katika mavazi yetu (ya Kiislamu), wale watakaowaitikia watatupwa motoni. Nilimuuliza Mtume s.a.w. unatuamuru nini katika hali hii? Alisema (katika hali hiyo) jiungeni na Jumuiya ya Waislamu yenye Imam mmoja. Nilimuuliza tena kwamba kama haitakuwapo Jumuiya wala Imam, tufanye nini? Alisema wacheni makundi na firka zote, na msijiunge mahali popote. Afadhali kuenda porini na kushika mizizi ya miti kwa meno mpaka kifo. *(Bukhari Kitabul Manaaqib. Mishkaat Baabul Fitan).*

Sasa alama zote za upotevu zimetimia. Waislamu wamegawanyika. Kweli kweli mambo yanafundishwa kinyume cha muongozo na suna za Mtume Mtukufu s.a.w. Katika hali hii amri ya Mtume Muhammad s.a.w. ni hii kwamba tujiunge na Jumuiya ya Waislamu yenye Imam mmoja. Kwa kweli katika siku hizi makundi ya Waislamu ni mengi lakini kundi lolote halina Imam kati yao kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Yaani ni magawanyiko tu, hakuna Jumuiya yoyote. Kwa sababu Jumuiya inahitaji Imam na bila Imam hawaitwi Jumuiya.

Kwa fadhili ya Mwenyezi Mungu Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya inayo Imam mmoja - Khalifa kutoka kwa Mwenyezi Mungu ambaye anaongoza Waahmadiyya wa duniani kote, na ndiyo Jumuiya pekee yenye sifa hii. Sisi tumefuata amri ya Mtume Mtukufu s.a.w. Tumejiunga chini ya Imam na kwa sababu hii tunaitwa Jumuiya . Tunawakaribisha wengine wote katika Jumuiya ya Waislamu yenye Imam mmoja kati yao.

Lakini kama hamtosheki na Jumuiya hii na Imam wake ilhali mnakosa Imam kutoka kwa Mwenyezi Mungu kati yenu, basi fuateni amri ya pili ya Mtume s.a.w. ya kuacha makundi yote na kwenda porini kushika mizizi kwa meno mpaka mauti yawafikie. Hii inamaanisha kwamba watu bila Imam hawana ruhusa kujiunga na kundi lolote la dini bali wajitenge na yote kwa kiasi hiki kwamba waishi porini na wafunge midomo yao

kuhusu mambo ya dini. Hawana ruhusa wala madaraka ya kuielezea dini kwa sababu ya kukosa Imam kati yao.

Siku hizi duniani kote ni Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya pekee iliyo na Imam na Khalifa kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Kwa njia hii siku hizi duniani kote Waahmadiyya pekee ndio wanaostahiki kuitwa Jumuiya ya Waislamu yenye Imam mmoja na ndio pekee wanaoruhusiwa kufanya kazi ya kuwaita watu kwa Mwenyezi Mungu. Kwa sababu hii tunawakaribisheni nyote katika Jumuiya ya Mwenyezi Mungu, ili tujenge na tupate umoja na udugu katika Dini ya Kiislamu. Tuachane na makundi bali tutulie chini ya bendera ya Mtume Muhammad a.s.w. ambaye ni Mtume wa walimwengu. Bendera ya Mtume Muhammad s.a.w. leo imeshikwa na mwanafunzi wake mtiifu Masihi Aliyeahidiwa - Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s.

**Swali:**
Kama mtu anataka kujiunga na Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya afuate utaratibu gani?

**Jibu:**
Ewe ndugu yangu kama wewe hujasilimu ni lazima kwako kwanza umtambue na umuamini Mwenyezi Mungu Mmoja na Mtume wake Mtukufu Muhammad s.a.w. Kuamini huko si kugumu bali ni kukubali kwa moyo na kukiri kwa ulimi kwamba hakuna apasaye kuabudiwa ila Allah na Muhammad ni Mtume wa Allah. Kutoa shahada hii inatosha kusilimu. Baada ya kusilimu Muislamu anawajibika kutenda vitendo kadhaa.

Na ewe ndugu yangu kama wewe tayari ni Muislamu basi kazi yako ni kumpokea Imam wa zama hizi. Kwa sababu Mtume Mtukufu s.a.w. amesema kwamba mtu ambaye amekufa bila kumtambua Imam wa zama zake, amefariki kifo cha ujinga (na ukafiri) (*Abu Daudi - Kanzul Umal* Jal 1 uk. 200.)
Katika Hadithi Nyingine Mtume s.a.w. amesema kwamba mtu ambaye amefariki bila ya kujiunga na Jumuiya au alijitenga na Jumuiya amefariki

kifo cha ujinga. *(Sahihi Muslim - Riyadhussalihiin* No. 668).
Na juu ya Imam Mahdi hasa Mtume s.a.w. aliagiza kwamba: Mtakapomuona mufanye Bai'at (ahadi ya utii) kwake hata kama itawabidi kutambaa juu ya theluji kwa sababu yeye atakuwa ni Khalifa aliyeongozwa na Mwenyezi Mungu *(Ibn Maajah, Kitaabul Fitan, Baabu Khuruujil Mahdiyyi).*

## AHMADIYYA NI NANI?

Baada ya kujiunga na Jumuiya tunawajibika kufuata kabisa Dini ya Kiislamu. Sayyidna Ahmad a.s. mwanzilishi wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya amesema kwamba:
"Kila mtu ambaye anafanya Bai't kwa mkono wangu ni lazima kwake ajue lengo la Baiat yake. Je anafanya Baiat kwa ajili ya dunia au kupata radhi ya Mwenyezi Mungu?
Wako wengi wenye bahati ndogo ambao lengo lao la kufanya Baiat ni dunia tu. Wala hayapatikani mabadiliko ndani yao baada ya kufanya Baiat, wala haipatikani nuru ya maarifa na yakini ya kweli katika dhati yao, na mambo haya mawili ni matokeo na matunda ya Baiat ya uhakika. Zaidi ya hayo hawaboreshi vitendo vyao wala hawajipambi wala hawasongi mbele katika mema. Pia hawajiepushi na maovu. Basi wajirekebishe ambao lengo lao ni dunia tu. Kwa hakika dunia hii ni ya siku chache, kisha ni kurejea kwa Mwenyezi Mungu Subhaanahuu wata'ala. Maisha haya ya muda mfupi yataisha kwa vyovyote, kwa dhiki au faraja. Lakini jambo la akhera ni la thamani sana. Kwa hakika akhera ni nyumba ya kudumu ambayo haitakatika.
Wakati mtu amehamia akhera na mambo yake ni safi na wazi kwa Mwenyezi Mungu na moyo wake umejaa hofu, na ametubu maasi na dhambi zote, wakati ule Mwenyezi Mungu anashika mkono wa mtu kwa rehema na fadhili zake. Kwa hivi mtu anapata radhi ya Mungu na anakuwa radhi naye.
Na kama mtu asifanye hivi bali aishi maisha ya kutojali, basi lazima akhera yake itakuwa mbaya sana".
(*Al Hakam* 17, Oct, 1902 uk. 2).

Sayyidna Ahmad a.s. ameeleza zaidi kwamba:

Msidhani kuwa mmefanya baiat kwa dhahiri kwani kukiri dhahiri si kitu. Mwenyezi Mungu anatazama mioyo yenu na roho zenu, na atawatendeeni sawa na hali ya mioyo yenu.

Tazameni! Mimi natimiza faradhi ya kubashiri baada ya kusema haya kuwa: Dhambi ni sumu msiile. Kumwasi Mwenyezi Mungu ni kifo kibaya kiogopeni: Ombeni ili mpewe nguvu. Sikilizeni, mtu asiyemfahamu Mwenyezi Mungu kuwa ana uwezo juu ya kila kitu wakati wa kuomba kwake hayumo katika jamaa yangu. Mtu asiyetanguliza dini juu ya dunia, kweli kweli, hayumo katika jamaa yangu. Mtu asiyeacha kila kitendo kibaya kama kunywa pombe na kucheza kamari na kutazama wanawake na kuzini na hiyana na rushwa, na kila jambo lisilojuzu kutenda na asiyetubia kutubu kwa kweli, hayumo katika jamaa yangu.

Mtu asiyedumu katika kusali sala tano siku zote hayumo katika jamaa yangu. Mtu asiyeshughulika katika kuomba kwa daima, wala hamkumbuki Mwenyezi Mungu siku zote kwa unyenyekevu hayumo katika jamaa yangu. Mtu asiyeacha rafiki mbaya mwenye kumwingiza mambo mabaya moyoni mwake hayumo katika jamaa yangu. Mtu asiyewaheshimu wazazi wake wala asiyezitii amri zao maarufu, zisizo kinyume cha Kurani Takatifu, wala hawatumikii kwa haki, hayumo katika jamaa yangu.. Mtu asiyemfanyia wema mke wake na jamaa za mke wake kwa upole na ihsani hayumo katika jamaa yangu. Mtu mwenye kumnyima jirani yake hata kheri kidogo, hayumo katika jamaa yangu.. Mtu asiyetaka kumsamehe mwenye kumkosea na mwenye kumbughudhi hayumo katika jamaa yangu. Kila mume mwenye kufanya hiyana kwa mke wake na kila mke mwenye kufanya hiyana kwa mume wake, hayumo katika jamaa yangu.

Mtu avunjaye ahadi aliyoahidi wakati wa kukiri na kuingia katika jamaa Ahmadiyya, kwa sababu yo yote, hayumo katika jamaa yangu. Mtu asiyeamini kwa kweli kuwa mimi ni Masihi na Mahdi aliyeahidiwa, hayumo katika jamaa yangu. Mtu asiyejiweka tayari kunitii katika mambo maarufu, hayumo katika jamaa yangu. Mtu anayekaa pamoja na watu

walionikataa na kukubali maneno yao ya upinzani hayumo katika jamaa yangu. Na kila, mzinzi, fasiki, mlevi, mwuaji, mwizi, mcheza kamari, haini, mla rushwa, mnyang'anyi, mdhalimu, mwongo, mhadaa na mwenye kukaa na watu hawa wote, na mwenye kusingizia ndugu zake na dada zake na asiyeacha vitendo vyake vibaya, wala asiyeacha kukaa na watu wabaya, hayumo katika jamaa yangu.

Kumbukeni kuwa haya yote ni sumu na baada ya kuzila sumu hizi hamwezi kusalimika. Nuru na giza haiwezekani kukusanyika pahali pamoja. Kila mtu mwenye tabia yenye kujikunja wala si safi kwa Mwenyezi Mungu hawezi kupewa baraka inayopewa wenye mioyo safi. Bahati gani nzuri ya wale wanaosafisha mioyo yao na kutakasa roho zao na kila uchafu na kufungamana na Bwana wao Mwenyezi Mungu ahadi ya uaminifu! Hawatapotezwa kabisa!! Haiwezekani Mungu kuwafedhehesha sababu wao ni wa Mwenyezi Mungu na Mwenyezi Mungu ni wa kwao. Nao wataepushwa na kila balaa. Ni mpumbavu adui yule ambaye awakusudia ubaya, kwa sababu wao wanabebwa na Mungu, yaani wamo katika ulinzi Wake". (Safina ya Nuhu Uk. 13-14).

Sayyidna Ahmad a.s. amesema kwamba:

Ni nani aliyeokolewa? Aliyeokolewa ni yule mwenye yakini kuwa Mwenyezi Mungu kweli yupo na Mtume Muhammad, amani ya Mungu juu yake, ni mwombezi katikati ya Mungu na viumbe vyake vyote. Na kuwa hapana Nabii ye yote aliye sawa na Mtume Muhammad, amani ya Mungu juu yake; na kuwa hapana kitabu cho chote sawa na Kurani Takatifu chini ya mbingu. Na Mungu hakupenda kwa ye yote awe mzima wa milele ila kwa Mtume huyu mtukufu aliye ni mzima wa milele, Yaani Mwenyezi Mungu kwa ajili ya kumweka mzima wa milele amefungua chemchem ya sheria yake na mibaraka ya utukufu wake kuendelea mpaka siku ya Kiyama. Na mwisho kwa baraka ya utukufu wake amemtuma duniani *Almasih-ul-Mau'ud* (Masihi Aliyeahidiwa) ambaye kuja kwake kulikuwa na lazima kwa kukamilisha jengo la dini ya

Kiislamu. Maana ilikuwa lazima kwamba dunia hii isiishe mpaka aje Masihi mmoja aliye kwa asili ya rohoni mfano wa Nabii Isa a.s., katika umati wa Muhammad, amani ya Mungu juu yake, kama ulivyopewa umati wa Musa a.s. (Safina ya Nuhu uk. 10).

Pia Hadhrat Ahmad a.s. amesema:

Hawezi kujiunga na Jumuiya yetu isipokuwa yule ambaye ameshaingia katika dini ya Kiislam, na anafuata Kitabu cha Mwenyezi Mungu na sunna za Mtume wetu Muhammad s.a.w. ambaye ni mbora wa viumbe vyote. Na anaamini Mwenyezi Mungu na Mtume wake ambaye ni mheshimiwa na mrehemu. Na anaamini siku ya kiyama na pepo na Jahannam, vile vile anaahidi na anakiri kwamba Dini yoyote haifai minghairi ya Mwenyezi Mungu na atakufa ndani ya dini hii iliyo dini ya asili, inayolengana na kitabu cha Mungu, mjuzi na anatenda sambamba na sunna na Quran na Ijmaa (kauli moja) ya masahaba. Na ambaye anaviwacha vitu hivi vitatu basi amejitupa motoni, na marejeo yake ni maangamio.
Basi ndugu zangu bila shaka imani haithibitiki ila kwa vitendo vizuri na kwa uchamungu. Mtu ambaye anawacha vitendo vizuri kwa kusudi na kwa kiburi basi hana imani mbele ya Mwenyezi Mungu.
Enyi ndugu zangu mcheni Mwenyezi Mungu na harakisheni kutenda mema na mjiepushe na maovu kabla ya kifo. (*Mawaahibu ur Rahman* uk. 13).

Iwapo unapenda kununua vitabu zaidi vya Dini ya Kiislamu au kwa maelezo zaidi ya mafundisho ya Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya, wasiliana na anuani iliyo karibu nawe kati ya hizi zifuatazo:

1. P. O. Box 376, Simu: 2110473 Dar es Salaam.
2. P. O. Box 1, Simu: 2603477 Morogoro.
3. P. O. Box 260, Simu: 2646849 Tanga.
4. P. O. Box 359 Iringa. Simu 2701782.
5. P. O. Box 196, Simu: 043043 Dodoma.
6. P. O. Box 94, Simu: 2600847 Songea.
7. P. O. Box 10723 Arusha. Simu 0741-273801
8. P. O. Box 54, Simu: 2603291 Tabora.
9. P. O. Box 547 Ujiji - Kigoma.
10. P. O. Box 306, Simu: 2333919 Mtwara.
11. P. O. Box 86, Simu: 2510082 - Masasi.
12. P. O. Box 1812 Bukoba.
13. P. O. Box 28, Simu 70 Kibiti - Rufiji.
14. P. O. Box 391 Tarime.
15. P. O. Box 605 Ifakara.
16. P. O. Box 17 Kilosa.
17. P. O. Box 833 / 3823 Zanzibar
18. P. O. Box 851 Mbeya
19. P. O. Box 47 Moshi (Machame)
20. P. O. Box 1203 Mwanza
21. P. O. Box 75 Nachingwea
22. P. O. Box 40554, Simu: 764226 Nairobi Kenya.
23. P. O. Box 97011, Simu: 492624 Mombasa Kenya.
24. P. O. Box 421, Simu 40269 Kisumu Kenya.
25. Private Bag 552 Limbe Malawi.
26. B.P. 3020 Bujumbura Burundi.
27. President Jamaat Ahmadiyya. Box Balama Village, Mozambique.

Hadhrat Abu Huraira r.a.amesimulia kwamba Mtume s.a.w. amesema: Hakika Mwenyezi Mungu atainua kwa ajili ya umati huu katika kila karne mtu wa kuijadidisha dini yao. (Abu Daud Kitaabul Malaahim).

Hadhrat Anas bin Malik r.a. amesimulia kwamba Mtume s.a.w. amesema: Hakuna Mahdi ila Isa
(Ibn Majaah, Kitaabul Fitan, Baabu Shiddatuz zamaan).

<u>Masihi wa Musa a.s.</u>
Mwenye rangi nyekundu, nywele zilizosokotana na mwenye kifua kipana. (Bukhari Kitaabul Ambiyaa).

<u>Masihi wa Muhammad s.a.w.</u>
Mwenye rangi ya ngano na mwenye nywele ndefu zilizonyooka. (Bukhari Kitaabul Libaas).

Kwa ajili ya wenye kutafuta ukweli tunaambatanisha hapa fomu ya Baiat ya kujiunga na Jumuiya ya Mwenyezi Mungu, sawa na masharti yake. Andikeni barua ya aina hii na baada ya kuweka sahihi uitume kwetu.

**MASHARTI YA KUINGIA KATIKA JUMUIYA YA WAISLAMU WAAHMADIYYA**

**Yaliandikwa na Seyyidna Ahmad, Mjumbe wa Mwenyezi Mungu.**

1. Mwenye kutaka kuingia katika Umoja huu uitwao Ahmadiyya ni juu yake kufanya ahadi kwa moyo wote ya kuwa hatamshirikisha Mwenyezi Mungu na chochote mpaka aingie kaburini.
2. Atajitahidi sana kujiepusha kabisa na kusema uwongo, wala hatatazama wanawake wala kufanya ufisadi, ufidhuli, hiyana na uasi, hatavikaribia vitendo vya namna hii, wala hatashindwa na tamaa mbaya za nafsi yake.
3. Atatekeleza Sala tano kwa nyakati zake hasa zilizowekwa kwa amri ya Mwenyezi Mungu na Mtume wake *s.a.w.* na zaidi ya hayo atajitahidi sawa na uwezo wake kusali sala ya Tahajjud na atamsalia Mtukufu Mtume Muhammad *s.a.w.,* na daima ataomba msamaha wa dhambi zake kwa Mwenyezi Mungu, na kwa shauku ya moyo wake ataikumbuka hisani ya Mwenyezi Mungu, na atamhimidi sana siku zote.
4. Tena hatawadhuru hususa Waislamu na kwa ujumla viumbe wote wa Mwenyezi Mungu kwa sababu ya tamaa mbaya ya nafsi yake, si kwa mkono wake wala kwa ulimi na viungo vyake vingine.
5. Atakuwa radhi juu ya kudra ya Mwenyezi Mungu katika kila hali ya taabu na raha, dhiki na faraja, msiba na neema. Kwa neno zima atakuwa tayari kukubali fedheha na maumivu katika njia ya Mwenyezi Mungu, naye atakapopata msiba wowote hatageuka bali ataendelea mbele kufuata amri yake Mungu.
6. Ataacha kabisa kufuata desturi mbaya ya kutii tamaa ya nafsi yake na kutii mila za watu; bali atakubali amri ya Mwenyezi Mungu na kauli ya Mtume Muhammad *s.a.w.* katika mwenendo wake siku zote.
7. Ataacha kufanya kiburi na majivuno na ataishi kwa tabia njema na huruma na atakaa kwa unyenyekevu, kwa adabu na upole sana.
8. Atafahamu dini na heshima yake na kazi ya Uislamu kuwa ni bora kuliko mali yake na heshima ya nafsi yake na kuliko watoto wake na wapenzi wake wote.
9. Atawahurumia daima viumbe wa Mwenyezi Mungu kwa ajili ya Mwenyezi Mungu tu, sawa na uwezo wake; naye atawaneemesha kwa zile neema alizopewa yeye na Mungu.
10. Katika ahadi ya udugu, atakayofungamana nami (Masihi niliyeahidiwa) kwa sharti ya kutii kila amri njema, atatimiza ahadi hii mpaka kufa kwake na katika ahadi hii ya udugu ataonesha utii na unyenyekevu wake kwa imara zaidi kuliko ufungamano wowote, wa damu au wa bwana na mtumishi.

(Tafsiri) ("Ishtehar Takmil-e-Tabligh" 12 Januari 89).

# AHADI YA BAI'AT

اَشْهَدُ اَنْ لَّا اِلٰهَ اِلَّا اللّٰهُ وَحْدَهٗ لَا شَرِيْكَ لَهٗ وَاَشْهَدُ اَنَّ مُحَمَّدًا عَبْدُهٗ وَرَسُوْلُهٗ

اَشْهَدُ اَنْ لَّا اِلٰهَ اِلَّا اللّٰهُ وَحْدَهٗ لَا شَرِيْكَ لَهٗ وَاَشْهَدُ اَنَّ مُحَمَّدًا عَبْدُهٗ وَرَسُوْلُهٗ

Nashuhudia ya kuwa hakuna apasaye kuabudiwa isipokuwa Mwenyezi Mungu. Yu Mmoja Asiye na mshirika. Na ninashuhudia ya kuwa Muhammad *s.a.w*. ni mtumishi Wake na Mtume wake.

Mimi leo najiunga na Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya kwa mkono wa **MASROOR AHMAD**. Nina imani kamili na thabiti kwamba Mtume Muhammad *s.a.w.* ni Mjumbe wa Mwenyezi Mungu na ni *Khaatamun Nabiyyiina.*

Mimi nakiri kuwa Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad wa Qadiani ndiye yule yule Imam Mahdi na Masihi Aliyeahidiwa ambaye bishara ya kuja kwake ilitolewa na Mtume Muhammad *s.a.w.* Mimi naahidi kwamba nitajitahidi kutekeleza masharti kumi ya Bai'at yaliyowekwa na Masihi Aliyeahidiwa *a.s.* Nitatanguliza dini juu ya dunia. Daima nitadumisha uaminifu wangu kwa Khalifa wa Kiahmadiyya na nitajitahidi kutekeleza maamrisho yake yote mema, kwa sababu ya kuwa kwake Khalifa wa Masihi.

اَسْتَغْفِرُ اللّٰهَ رَبِّيْ مِنْ كُلِّ ذَنْبٍ وَّاَتُوْبُ اِلَيْهِ ۞ اَسْتَغْفِرُ اللّٰهَ رَبِّيْ مِنْ كُلِّ ذَنْبٍ وَّاَتُوْبُ اِلَيْهِ ۞ اَسْتَغْفِرُ اللّٰهَ رَبِّيْ مِنْ كُلِّ ذَنْبٍ وَّاَتُوْبُ اِلَيْهِ

Ninamuomba Allah Mola wangu, msamaha wa dhambi zangu zote na ninatubu / naelekea Kwake.

رَبِّ اِنِّيْ ظَلَمْتُ نَفْسِيْ وَاعْتَرَفْتُ بِذَنْبِيْ فَاغْفِرْ لِيْ ذُنُوْبِيْ فَاِنَّهٗ لَا يَغْفِرُ الذُّنُوْبَ اِلَّا اَنْتَ

Ee Mola wangu, hakika mimi nilijidhulumu nafsi yangu na ninakiri dhambi zangu zote.
Nakuomba unisamehe dhambi zangu, kwani hakuna awezaye kusamehe dhambi isipokuwa Wewe. Amin.

## MAELEZO KAMILI YA WANAOJIUNGA

1. Jina ............................................ Tarehe ya kuzaliwa / umri .................

Raia ................................ Anuani ..............................................................

Masomo ........................... Kazi ....................... Sahihi .....................

Pia orodhesha majina ya watu wa familia walio chini ya uangalizi wako.

# THE MUSLIM JAMAAT WITH IMAM

**BY**

**SHEIKH MUZAFFAR AHMAD DURRANI**

This is a book written in Swahili language.
It covers the following topics:

1. The reason to start a new Jamaat.
2. The name of Ahmadiyya Muslim Jamaat.
3. Differences between Ahmadiyya Muslims and other Muslims.
4. Importance to join Ahmadiyya Muslim Jamaat.

For more information please contact the following address.

Ahmadiyya Muslim Jamaat
P. O. Box 376 Dar es Salaam
Tel: 022 - 2110473 Fax 022 - 2121744

Printed by:
Ahmadiyya Printing Press
Dar es Salaam